

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania  
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA DAR ES SALAAM (“DAWASA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22**

### **Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TRW-18-054**

Mnamo tarehe 28 Februari 2019 EWURA ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ya kuendelea kutumia bei ya mpito iliyoidhinishwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, na ambayo muda wake utakwisha ifikapo tarehe 30 Juni 2019.

Jedwali namba 1 (a) to (c) hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

### **BEI NA ADA ZA SASA NA ZINAZOPENDEKEZWA**

#### **Jedwali 1(a): Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa za Maji (Shilingi/Uniti)**

	<b>Bei za Sasa</b>	<b>Bei Inayopendekezwa</b>
	<b>2018/19</b>	<b>2019/20 mpaka 2021/22</b>
<b>Bei ya Mteja</b>	<b>1,663</b>	<b>1,663</b>

#### **Jedwali 1(b): Bei ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kuondoa Majitaka (TZS/m<sup>3</sup>)**

	<b>Bei za Sasa</b>	<b>Bei Inayopendekezwa</b>
	<b>2018/19</b>	<b>2019/20 mpaka 2021/22</b>
<b>Bei ya Mteja</b>	<b>386</b>	<b>386</b>

**Jedwali 1(c): Gharama Zingine za Sasa na Zilizoidhinishwa**

Aina ya Gharama	Gharama za Sasa	Gharama zinazopendekezwa
	2018/19	2019/20 mpaka 2021/22
Amana ya Dira	50,000	50,000
Ada ya Maunganisho mapya ya	26,000	26,000
Ada ya Kurejeshewa Huduma - wateja wa majumbani	15,000	15,000
Ada ya Kurejeshewa Huduma - wateja wa majumbani	16,000	16,000
Gharama za kumwaga majitaka	1,000	1,000
Bei ya jumla ya maji	1,106	1,106
Bei ya Magati	1,106	1,106

Kwa mujibu wa wasilisho la DAWASA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji na uwekezaji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 19 Juni, 2019, katika mji wa Bagamoyo na katika mji wa Kibaha na Alhamisi tarehe 20 Juni 2019 katika jiji la Dar es salaam.** Mikutano yote hii itafanyika kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwu hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **21 Juni, 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA PSSSF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa DAWASA zilizopo Mwananyamala Dar es Salaam, Mkabala na Hospitali ya Mwananyamala Dar es Salaam.

**Imetolewa na  
Kaimu Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)  
31 Mei 2019**